



# KENYA PRIVATE SCHOOLS ASSOCIATION GREDI LA 5

Jaribio la kati Muhula wa Kwanza - 2021  
KISWAHILI: Sehemu ya Kwanza - Lugha

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

GREDI \_\_\_\_\_

TAREHE \_\_\_\_\_

## ZOEZI: I - KUSOMA KWA UFAHAMU

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 7*

Mipango yote ya sherehe ya kuzaliwa kwa baba yangu ilikuwa imepangwa ikapangika. Ilikuwa siku ya tatu ya juma. Baba alikuwa akikamilisha miaka thelathini na tisa. Yeye hakuwa amekula chumvi nyingi kama alivyokuwa babaye Meishisana.

Mapochopocho ya vyakula mbalimbali yalikuwa yakinukia mezani na hata mekoni. Vyakula kama vile pilau, biriani, maandazi na vibanzi vilivutia sana machoni pa wageni watano waalikwa. Nilishangaa nilipomwona Bwana Kauleni akidondokwa na mate kwa sababu ya kuitamani keki yenyewe. Watu wengine ambao sikuwatambua kwa majina yao, walikuwa wameketi kitako sebuleni huku wamejipamba kweli kweli. Bila shaka wote walijawa na tabasamu nyusoni pao.

Keki yenyewe ilikuwa tamu kama halua. Mimi mwenyewe nilihusika kwa kuwakaribisha marafiki zangu kwenye viti baada ya kuvipanga.

### Maswali

1. Je, kisa hiki kinahusu sherehe ya nani? \_\_\_\_\_
  2. Sherehe yenyewe ilikuwa siku gani ya juma? \_\_\_\_\_
  3. Mwandishi alitumia maneno, "hakuwa amekula chumvi nyingi." Je, hii inamaanisha nini? \_\_\_\_\_
  4. Wageni walikuwa wameketi kitako. Pigia mstari kielezi katika sentensi hii.
  5. Je, sherehe hii ilihudhuriwa na wageni wangapi waalikwa? \_\_\_\_\_
  6. Taja jina la babaye mwandishi \_\_\_\_\_
- Kifungu ulichokisoma kinahusu nini? \_\_\_\_\_

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 8 hadi la 14.*

Mwaka huu ulipoanza, sote tulifurahi kurudi katika shule yetu. Shule hiyo inajulikana kama Mematele. Ina wanafunzi elfu moja na mia mbili na mabasi sita. Mabasi yote ya shule hiyo yamepakwa rangi ya manjano.

Tulipowasili shuleni, tuliingia madarasani na kuketi kwenye viti vyetu. Mwalimu mmoja ambaye tulimpenda sana aliingia darasani na kutuamkua, "Hamjambo wanafunzi?" Nasi tukajibu, "Hatujambo mwalimu Matunda. Shikamoo."

Kengele ilipopigwa tulielekea gwarideni. Tulisimama wima tulipokuwa tukiimba wimbo wa taifa. Baadaye mwalimu alitukagua endapo kucha zetu zilikuwa safi. Mwalimu wetu alitushauri tuwe tukinywa maji mengi kila siku ili tuwe na afya njema.

### MASWALI

8. Malizia sentensi hii.  
Mwaka huu ulipoanza sote tulifurahi .....
9. Mwandishi husomea katika skuli gani? \_\_\_\_\_
10. Shule ya mwandishi ina wanafunzi wangapi? \_\_\_\_\_

11. Mabasi ya shule katika nchi hii ya msimulizi yamepakwa rangi gani? \_\_\_\_\_
12. Salamu hamjambo hujibiwa hatujambo je, masalheri hujibiwa aje? \_\_\_\_\_
13. Ni nani aliwashauri wanagenzi kunywa maji mengi? \_\_\_\_\_
14. Kwa nini wanafunzi walishauriwa kunywa maji mengi? \_\_\_\_\_

## ZOEZI II - SARUFI

15. Teua salamu ambayo haijaambatanishwa ipasavyo.

Habari ya jioni..... njema  
Kwa heri ..... ya kuonana  
Alamsiki..... aleikum salaam  
Makiwa ..... tunayo \_\_\_\_\_

16. Je, kati ya maneno haya katika kamusi, ni neno gani litakuwa la pili?

Muhubiri, Muhutasari, Muhula, Mtihani, Mshtakiwa \_\_\_\_\_

17. Mstatili huu una maneno matano ya nomino za vitenzi-jina. Je, ni neno lipi halifai kuwa hapa?

Kulala, Kukimbia, Kalia, Kusoma, kutibiwa

**Andika kwa wingi.**

18. Mtoto aliacha dawati lake shuleni. \_\_\_\_\_
19. Mwalimu wangu huja mapema shuleni \_\_\_\_\_
20. Chagua neno sahihi kujaza nafasi: Matata \_\_\_\_\_ nyanya samaki. (alibeba, alimbebea, alimbeba)

**Chagua neno lifaalo kujaza nafasi.**

21. Tulienda sokoni \_\_\_\_\_ kununua matunda. (ili, kwa sababu)
22. Kamilisha methali hii. Asiyekujua \_\_\_\_\_ {akuthanini, hakuthamini, hakudhamini}

**23. Ni sentensi gani haijakanushwa vyema?**

Tunaenda sokoni	Hatuendi sokoni
Mama yangu amechelewa	Mama yangu hachelewi
Walionana mwaka jana	Hawakuonana mwaka jana.
Juma ni mwanafunzi hodari	Juma si mwanafunzi hodari

Nomino, "jua, lepe, jasho, joto na giza," hupatikana katika ngeli ya \_\_\_\_\_

25. Andika sentensi hii katika hali ya ukubwa

Mtoto wake anasoma. \_\_\_\_\_

**Je, sentensi hii iko katika wakati gani?**

26. Mlinzi mwenyewe analilinda rinda la mama. \_\_\_\_\_
27. \_\_\_\_\_ (Karamu, Ghulamu, Kalamu) ya arusi ilikuwa ya kupendeza sana.

Siku hiyo \_\_\_\_\_ 28 \_\_\_\_\_ (pipi, vivi, bibi) arusi alivaa gauni jeupe pe pe pe.

Jaza mianya iliyoachwa kwa maneno yafaayo kutoka kwenye duara dufu **Shule, mwiko, vitunguu, sabuni**

29. Mama alipokuwa akisonga ugali alitumia \_\_\_\_\_

30. Idadi ya wanafunzi katika \_\_\_\_\_ yetu ni elfu mbili.